Maswali Yanayoulizwa Sana

Je, ni maeneo gani ya hifadhi, burudani ambayo yamefunguliwa?
Kufikia Juni 4, maeneo mengi ya umma yanayosimamiwa na jimbo yalikuwa yamefunguliwa tena kwa **matumizi ya mchana**.

Shughuli za kupiga kambi zinafunguliwa tena katika kaunti nyingi ambazo zimehamia Awamu ya 2 ya mpango wa Gavana Jay Inslee wa Safe Start (Uanzishaji Salama).

Maeneo ya kushua boti wazi na bandari zinazosimamiwa na jimbo katika hifadhi za jimbo kwenye kaunti zilizo katika Awamu ya 2 zimefunguliwa pia.

Ili kujua hali ya sasa ya viwanja vya kambi, hifadhi na maeneo mengine ya burudani yanayosimamiwa na jimbo tembelea:

- Washington State Parks - Hali ya hifadhi
- Washington Department of Fish and Wildlife - Orodha ya kufungwa na vizuizi
- Washington State Department of Natural Resources - Kufunguliwa kwa maeneo ya burudani

Kumbuka: Baadhi ya hifadhi kwenye kaunti zilizo katika Awamu ya 2 **huenda zisifunguliwe** mara moja kwa shughuli za kupiga kambi, kwa kuzingatia maelekezo kutoka kwa maafisa wa kaunti. Washington State Parks zinasaidia na zinaendelea kushirikiana na jamii hizi ili kupata mbinu bora ya kufungua tena shughuli za kupiga kambi.

Je, ninahitaji Discover Pass?
Ndiyo. Discover Pass inahitajika ili uegeshe gari lako katika maeneo ya burudani na maeneo ya ufikiaji wa maji yanayosimamiwa na Washington State Parks na Department of Natural Resources (DNR). Maeneo haya ni pamoja na hifadhi, maeneo ya ufikiaji wa maji, maeneo ya utamaduni, maeneo ya wanyama pori na maeneo ya asili, viwanja vya kupiga kambi vya DNR, vijia na sehemu ambapo vijia huanzia na maeneo yote ya vilima yanayosimamiwa na DNR. Discover Pass inahitajika katika hifadhi za jimbo kwa ziara za matumizi ya mchana tu.

Discover Pass pia inahitajika katika maeneo yanayosimamiwa na Washington Department of Fish and Wildlife (WDFW). Haya ni pamoja na maeneo ya ufikiaji wa maji na maeneo ya wanyama wa pori, isipokuwa kama tayari una Vehicle Access Pass iliyotolewa pamoja na ununuzi wa leseni halali ya uwindaji au uvuvi.

Je, ninaweza kuongezewa muda au kurejeshewa pesa kwenye Discover Pass kwa wakati ambao maeneo ya jimbo yalikuwa yamefungwa?
Haturejeshi pesa wala hatuongezi muda wa Discover Passes.

Discover Pass ya kila mwaka inagharimu $30. Bei ya pasi ya siku ni $10, kwa hivyo gharama ya pasi ya mwaka huwa inajilipa katika ziara tatu tu.

Ukigawanya na miezi 12, gharama ya kila mwezi ni $2.50. Maeneo ya jimbo yalifungwa kuanzia Machi 23 hadi Mei 5, muda uliozidi wiki tano kidogo.

Hifadhi za Jimbo zimepata hasara kubwa za mapato katika msimu huu wa masika – pamoja na punguzo katika ufadhili kutoka hali iliyopita ya Kudorora Sana kwa Uchumi.

Hata hivyo, tunawasihi ufurahie hifadhi na maeneo ya jimbo la Washington mara nyingi katika msimu huu wa kiangazi na zaidi ili upate thamani kubwa inayowezekana kutoka kwa pasi yako.

Je, viwanja vya michezo vimefunguliwa?
Viwanja vya michezo vya Hifadhi za Jimbo vimefungwa mpaka itakapotangazwa vinginevyo ili kupunguza maambukizi ya COVID-19.

Je, misala imefunguliwa?
Ndiyo. Katika hifadhi ambazo zimefunguliwa, misala itapatikana katika maeneo yanayofunguliwa wakati wa mchana na na maeneo ambayo shughuli za kupiga kambi zimefunguliwa. Huenda misala ikafungwa katika baadhi ya maeneo na katika viwanja wa kambi vilivyofungwa.

Kuwa tayari. Tafadhali kuwa na vifaa vyako vya kibinafsi vya kinga, maji, sabuni, sanitaiza ya mikono na karatasi ya chooni, na urudi nyumbani na bidhaa hizi.

Ofisi za Hifadhi bado zimefungwa kwa umma, vile vile vituo vya wageni na majengo ya hifadhi.

Je, bandari, fukwe na vituo vya hifadhi ya baharini vimefunguliwa?
Matumizi ya bandari yanaruhusiwa, na fukwe zinapatikana katika hifadhi ambazo zimefunguliwa. Watu wanaotumia bandari wanapaswa kudumisha umbali wa kutengana na watu wengine ambao sio sehemu ya familia yao.

Misala ya hifadhi za baharini za jimbo itafunguliwa kwa muda mchache. Tafadhali rudi nyumbani na taka zako, na usitarajie maji ya kunywa katika visiwani.

Je, shughuli za kutia nanga zitafuatiliwa au kudhibitiwa? Na, je, itakuwaje kwa maeneo ya kutua kwa pwani kwa kihori?
Shughuli za kutia nanga zitafuatiliwa na kudhibitiwa kama ilivyokuwa kabla ya kufungwa kutokana na COVID-19. Hakuna sheria maalum zilizowekwa.

Je, huduma za kuondoa uchafu kutoka kwa boti zimefunguliwa na zinafanya kazi?
Huduma kadhaa za kuondoa uchafu zilizo ndani ya hifadhi ya jimbo zimefunguliwa.

Huduma nyingi za kuondoa uchafu wa boti katika Washington zinapatikana kwenye bandari za umma au kibinafsi. Waendeshaji wa boti wanapaswa kuangalia katika bandari kujua kama wamefungua na iwapo huduma za kuondoa uchafu wa boti zinafanya kazi. Kwa maeneo ya huduma za kuondoa uchafu wa boti katika Washington, tembelea: parks.state.wa.us/657/Pumpout

Ikiwa hifadhi inafunguliwa tu kwa matumizi ya mchana, je, hifadhi itakuwa inafungwa saa ngapi?
Hifadhi za matumizi ya mchana zinafunga wakati wa magharibi.

Je, nitarejeshewa pesa kamili kwa kambi au uwekaji nafasi wa malazi ya usiku mmoja?
Inategemea…

- **Wageni wa usiku walioathirika na kufungwa:** Tunawasiliana na wageni wa usiku ambao uwekaji wao wa nafasi umeathiriwa na kufungwa ili kutoa marejesho kamili.
- **Wageni kwenye hifadhi za kambi ambazo zimefunguliwa** wanaweza kurejeshewa malipo kamili kwa kukaa usiku, ukiondoa ada mbili za miamala ambazo haziwezi kurejeshwa (ada ya $8 hadi $10 ya uwekaji nafasi na ada ya $8 hadi $10 ya kughairi). Ada ya uwekaji nafasi ni $8 ikiwa uliufanywa mtandaoni na $10 ikiwa uliufanywa kupitia kwa simu.

Iwapo una swali kuhusu uwekaji nafasi wako wa sasa wa kambi, tafadhali piga simu (888) CAMPOUT au (888) 226-7688.

Je, itakuwaje endapo nina uwekaji nafasi katika hifadhi ambayo kwa sasa imefungwa kwa kupiga kambi? Nitajua lini ikiwa nafasi yangu imeghairiwa?
Tunakushukuru kwa uvumilivu wako tunaposhughulika hali hii inayobadilika. Tunajua mipango yako ya likizo ni muhimu, na tunatumai kuwa utaweza kupiga kambi katika hifadhi unayopendelea ya hifadhi za jimbo la Washington wakati wa msimu wa kiangazi.

Kwa sababu hiyo, tumesita kughairi nafasi zilizowekwa mpaka wakati tutakuwa na uhakika kabisa kuwa hifadhi haitafunguliwa tena kwa upigaji kambi kabla ya tarehe uliyoweka nafasi. Kwa hivyo, tunaweza kukosa kuwasiliana nawe hadi siku chache kabla ya wakati wako wa ziara.

Iwapo tunahitaji kughairi uwekaji nafasi katika hifadhi ambayo imeendelea na kufungwa kwa kambi, tutawasiliana nawe kwa barua pepe, na utarejeshewa pesa zote.

Kwa maswali mahususi kuhusu uwekaji wako wa nafasi, tafadhali wasiliana na timu yetu ya uwekaji nafasi katika 888-CAMPOUT (888-226-7688).

Je, maeneo ya jimbo yatafungwa iwapo kuna maswala ya kuwepo kwa watu wengi?
Tunapofungua tena maeneo, tunawaomba watu waendelee kudumisha umbali wa kutengana. Iwapo tutagundua kuwa vikundi vikubwa vinakusanyika au watu hawadumishi umbali wa kutengana, tunaweza kulazimika kuzingatia kufunga hifadhi au maeneo ndani ya hifadhi.

Iwapo kutaibuka wasiwasi mpya wa usalama unaohusiana na COVID-19, Washington Departments of Fish and Wildlife (WDFW) na Natural Resources (DNR) na Hifadhi za Jimbo zinaweza kufunga maeneo kwa taarifa ya haraka ili kulinda afya na usalama wa umma.

Je, ninawezaje kuripoti maswala yoyote ya kuwepo kwa watu wengi, takataka au wasiwasi wowote wa maeneo ya wanyamapori au kushua boti kwa WDFW?
Watu wanaweza kuripoti masuala kwenye tovuti ya Washington Department of Fish and Wildlife.

Je, ninaweza kujitolea kusaidia kusafisha na kutunza hifadhi ya jimbo katika eneo nilipo?
Sio kwa wakati huu. Tunawathamini wafanyakazi wetu wa kujitolea na saa zao za kazi ngumu. Hata hivyo, hakuna shughuli za kujitolea zitakazofanyika mpaka itakapotangazwa vinginevyo. Hifadhi za Jimbo zinajitahidi ili kuanza tena mpango wa kujitolea kuwa mwenyeji wa kambi na mipango mingine ya kujitolea baadaye katika msimu huu wa kiangazi. Angalia taarifa au wasiliana na Volunteer Program kwa barua pepe au piga simu (360) 902-8583.

Je, vibanda na yurt zitafunguliwa lini?
Vibanda, yurt na malazi ya kishamba bado zimefungwa kwa uwekaji mpya wa nafasi hadi Juni 30. Kwa vibanda vinavyoweza kufunguliwa mnamo Juni, nafasi zilizopo zitaruhusiwa kutumika.

Je, viwanja vya kambi vya vikundi vimefunguliwa?
Shughuli za kambi za vikundi zimefungwa mpaka itakapotangazwa vinginevyo.

Je, nyumba za likizo zimefunguliwa?
Nyumba za likizo zimefungwa mpaka itakapotangazwa vinginevyo.